MAMLAKA YA USIMAMIZI WANYAMAPORI TANZANIA

MWALIKO WA KUSHIRIKI MNADA WA MAENEO YA UWINDAJI WA WENYEJI NA WAGENI WAKAZI KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI

(Imefanyika chini ya kifungu cha 8 ya Sheria Uhifadhi Wanyamapori Na.05 ya mwaka 2009 kwa kuzingatia Kanuni ya uwindaji wa wenyeji ya mwaka 2021)

Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzanai (TAWA) inapenda kuwakaribisha Watanzania wenye sifa kuleta maombi yao kwa ajili ya kushiriki mgawo wa maneo ya uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi utakaoendeshwa kwa njia ya mnada ambayo yanapatikana kwenye Mapori Tengefu na maeneo ya wazi yenye wanyamapori (Open Areas). Kampuni stahiki hazitaruhusiwa kupata mgawo wa zaidi ya eneo moja kati ya maeneo yaliyotangazwa kwa mujibu wa sheria kupitia tangazo la Serikali la Na. 664 ya mwaka 2018 na Na. 691 ya mwaka 2019. Mnada unatarajiwa kufanyika tarehe 16 hadi 22 August, 2021 na utakamilika kwa muda wa siku saba kwa mfuatano.

1. SIFA ZA KUGAWA MAENEO YA UWINDAJI WA WENYEJI NA WAGENI WAKAZI

Kwa kuzingati Sheria Uhifadhi Wanyamapori sura ya 283 ya mwaka 2009 inataja kuwa mtu hatakuwa na sifa ya kupata eneo la uwindaji wa wenyeji isipokuwa;

a) Awe Mtanzania mwenye kumiliki Kampuni ambayo limesajiliwa kisheria Mtanzania mwenye dhamira ya kuwinda wanyamapori kupitia uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi.

b) Angalau mmoja wa Wakurugenzi wake awe na uzoefu usiopungua miaka mitano katika tasnia ya uwindaji wa wanyamapori.

c) Kampuni kuwa na sifa zilizobainishwa kwenye kanuni ya 5(2) ya kanuni ya uwindaji wa wenyeji ya mwaka 2021.

d) Mwombaji asiwe mmiliki wa kitalu chochote cha uwindaji wa kitalii hapa nchini.

e) Mwombaji anatakiwa kuwa Mtanzania.

2. SIFA ZA MWOMBAJI WA ENEO LA UWINDAJI WA WENYEJI

Mwombaji wa maeneo ya uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi, maombi yake yanalazimika kuzingatia vigezo vifuatavyo;

a) Awe na jengo la ofisi lenye hadhi kwa shughuli za biashara ya uwindaji
b) Awe na angalau gari moja 4WD aina ya pick up
c) Awe na vifaa vya mawasiliano vya uhakika
d) Awe angalau na Mahema mawili (tents) kwa ajili ya kupiga kambi
e) Awe na angalau jokofu moja na friji moja

3. **MUDA WA KUMILIKI VITALU**

a) Taarifa ya ukaguzi na tathimini itakayo kuwa ikifanyika kwa kila mwaka katika eneo atakalokuwa akimiliki na kuwindisha kwa kipindi cha miaka mitatu.
b) Uchambuzi wa kina wa kampuni zote za uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi utafanyika ili kuangalia uhalali wa kuhaulisha baada ya muda wa umiliki wa eneo la uwindaji kwa **miaka mitatu** kuisha.

4. **UTARATIBU WA MAOMBI NA MAELEKEZO**

a) Waombaji watakamilisha usajili wa maombi yao online kupitia tovuti https://portal.maliasili.go.tz kupitia form itayotolewa ya kielektronia(e-form).usajili utakaofanikiwa,jina litakalotumika kwenye mfumo pamoja na namba ya siri zitatumwa kupitia barua pepe itakayokuwa imesajiliwa ili kuwawezesha waombaji kuingia kwenye mnada wa kielektronia (e-auction Portal) na maelekezo ya namna ya kushiriki kwenye mnada ingia kwenye **youtube channel** ya **MNRT Portal**
b) Mwombaji hatakiwi kuchagua zaidi ya eneo moja kati ya maeneo yaliyotangazwa kwa ajili ya uwindaji kwa ajili ya kushindania zabuni ambayo itatoa moja kwa moja hati ya madai (e-invoice) kwa mwombaji kulipia kiasi husika na pesa hiyo haitarudishwa endapo mwombaji atashindwa zabuni (angalia jedwali hapa chini).Waombaji watatakiwa kulipa ada ya maombi ya eneo la uwindaji wa wenyeji kiasi cha shilingi laki mbili (200,000/=) kwa kila moja.
c) Waombaji watakaofanikiwa kulipa Ada ya ushiriki ndiyo watakaoruhusiwa kushiriki mnada kwa njia ya kielektronia ambao utakuwa wazi kwa muda wa siku saba za kufuatana.
a) Mshiriki katika mnada huo atatumia jina la usajili (surname) na neno la siri (password) ili kumwezesha kushiriki zabuni hiyo na atatakiwa kushiriki zoezi hilo kwa kuzingatia maelekezo kutoka kwenye mfumo wa zabuni husika.

b) Mshiriki wa zabuni atabaki kuwa siri kwa kipindi chote ambapo mnada utakuwa unaendelea.

Washiriki wote wa zabuni watatakiwa;

c) Kutoa na kamilisha ada ya eneo la uwindaji ambalo bado halijachaguliwa,
d) Logi kwenye mfumo wa e-auction zaidi ya mara moja wakati wa kushiriki zabuni,
e) Mshiriki atataarifiwa moja kwa moja zabuni mpya sambamba na bei husika, ambayo itawawezesha wanaoratibu kujua daraja lake wakati wa zoezi la kushiriki,
f) Vitambulisho vya washiriki havitatolewa wazi kwa upande wowote wa washiriki wakati zoezi la mnada,
g) Zabuni zitakazowasilishwa ambazo hazina uhalali zitakataliwa kwa ujumbe utaoeleza sababu za kukataliwa kwake,
h) Wazabuni wote hawatatakiwa kutoa taarifa za ziada au maelezo yoyote yanayohusu mnada ambao unaweza kuharibu zoezi la ushindani na kama italazimika basi taarifa hizo zitatolewa na TAWA,
i) Watumiaji wote watalazimika kutunza siri ya taarifa zote zinazohusiana na akaunti zao katika mfumo wa e-auction,
j) Mshindi atapatikana kupitia mfumo wa e-auction ambao utakuwa umezingatia bei ya ushindani, mgawo utazingatia mzabuni aliyetoa dau kubwa kati ya washiriki kwenye mnada husika.
k) Hakuna zabuni itayojiondoa baada ya hatua zote za zabuni kukamilika,
l) Mzabuni atakubaliwa kuongeza dau/bei ya wakati wa kushiriki zoezi la mnada,
m) Mzabuni aliyefaulu atalazika kulipa asilimia 25% ya bei ya juu iliyofikiwa ndani ya masaa 12 ya kazi baada ya kufungwa kwa mnada,
n) Kiasi cha kilichobaki cha asilimia 75% mshindi atalazimka kuwa amelipa ndani ya siku 14 kutoka tarehe ya kufungwa kwa mnada, kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kufutwa kwa umiliki huo na kiasi cha asilimia 25% ya ada iliyolipwa itataifishwa.
o) Mzabuni aliyefaulu atalazimika kulipa Ada ya eneo la uwindaji kwa kila mwaka kwa mujibu wa Muongozo wa uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi(2021) nje ya bei ya zabuni aliyoshinda.

ANGALIZO:

Mzabuni aliyefaulu tu ndiye atapewa cheti cha mgawo wa eneo la uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi na Kamishna wa Uhifadhi. Endapo unahita taarifa au maelezo ya ziada, tafadhali usisite kufanya mawasiliano ama tembelea ofisi zetu kwa msaada.

1. Kamishna wa Uhifadhi,
   Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania,
   Barabara ya Dar es Salaam -Eneo la Kingolwira,
   Jengo la Makao makuu ya Taaisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) ,
   S.L.P 2658,
   MOROGORO -Tanzania
   Tel: +255 23-293424
   E-mail: cc@tawa.go.tz
2. e-Auction of Hunting Blocks Help Desk Tanzania Wildlife Management Authority Phone: +255 784 878662; +255 717 187 156; +255 754 043 280
   E-mail: e-auctionhuntingblocks@tawa.go.tz

MAENEO YA UWINDAJI WA WENYEJI YALIYOPO KWENYE MNADA

SN	WILAYA	KITALU	HADHI	UKUBWA ($km^{2)}$	ECOSYSTEM	KANDA
1	Kilwa	Kilwa Open Area North	OA	1,758	Selous-Mikumi	Kusini
2	Kisarawe	Kisarawe Open Area	OA	1,292	Selous-Mikumi	Nyanda za Juu Kusini
3	Kilombero	Matundu Forest Reserve	FR	524	Selous-Mikumi	
4	Kiteto	Talamai Open Area	OA	2,677	Handeni-Kitwai	Kaskazini
5	Manyoni	Simbanguru/lgwamadate	OA	453	Ruaha-Rungwa	Kati
6	Sikonge	Ipemba Mpazi Open Area	OA	1,285	Katavi-Rukwa	

Ufunguo: OA = Open Area
FR = Forest Reserve

Imetolewa na:

Kamishna wa Uhifadhi,
Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA
Barabara ya Morogoro- Eneo la Kingolwira,
Jengo la TAFORI,
S.L.P 2658,
Morogoro - Tanzania.
Simu: +255 (0) 23-293424
Barua pepe: cc@tawa.go.tz